



RIPOTI YA KIHAIIDROLOJIA JARIDA LA MWEZI

BWAWA JULIUS NYERERE (JNHPP)

Agosti, 2026

Tarehe ya Utekelezaji: 24 Nov 2025
Toleo, No: 00




"KILA TONE LINATHAMANI"

Tarehe ya Utekelezaji: 24 Nov 2025
Toleo, No: 00

Muhtasari wa Hali ya Maji

Kituo cha Kuzalisha Umeme kwa Maji cha Julius Nyerere (JNHPP), kilichopo Stiegler's Gorge katika Mto Rufiji, Tanzania, hupokea maji kutoka katika mito mikuu mitatu ya Bonde la Rufiji: Great Ruaha, Kilombero na Luwegu. Mito hii hutoa maji yanayohitajika kwa uzalishaji wa umeme pamoja na matumizi ya kilimo, majumbani, viwandani, mifugo na mahitaji ya kimazingira.

Mwisho wa Agosti 2026, jumla ya mtiririko wa maji kutoka katika mito hiyo mitatu kwenda kwenye bwawa la JNHPP iliripotiwa kuwa asilimia 106% juu ya wastani wa muda mrefu wa mwezi huo. Hali hii iliathiriwa kwa kiasi kikubwa na mtiririko endelevu wa maji kutoka maeneo ya juu ya vyanzo vya maji pamoja na usimamizi madhubuti wa rasilimali za maji katika Bonde la Rufiji.



Hali ya Hewa

Hali ya Mvua – Agosti 2026:


Takwimu za mvua zinaonesha kuwa maeneo mengi ya Bonde yalikuwa na hali ya ukavu katika kipindi chote cha Agosti 2026. Kutokana na hali hiyo, maji yaliyotiririka juu ya uso wa ardhi yalikuwa machache, hivyo kusababisha kupungua kwa mtiririko wa maji katika mito na vijito, hususan vile vinavyotegemea mvua za msimu.

Mwelekeo wa Hali ya Hewa – Septemba 2026:


Kwa mujibu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), mvua nyepesi hadi za wastani zinatarajiwa katika maeneo mbalimbali ya Bonde la Rufiji wakati wa Septemba 2026. Mgawanyo wa mvua kwa wiki unaoneshwa katika taarifa unaashiria kuwa upatikanaji na mtawanyiko wa mvua utatofautiana katika maeneo mbalimbali ya bonde.

Wiki ya Kwanza	Wiki ya Pili	Wiki ya Tatu	Wiki ya Nne
Mvua nyepesi hadi mvua katika maeneo ya kati na mashariki	Mvua nyepesi hadi mvua katika maeneo ya kati na mashariki	Mvua nyepesi hadi mvua katika maeneo ya kati na mashariki	Mvua nyepesi


Utabiri wa Mvua
Wiki 01 Septemba, 2026




Utabiri wa Mvua
Wiki 02 Septemba, 2026



Utabiri wa Mvua
Wiki 03 Septemba, 2026



Utabiri wa Mvua
Wiki 04 Septemba, 2026




Hali ya Mtiririko wa Maji

Vituo vya Kihaidrolojia

Wastani wa mtiririko wa mito katika Agosti 2026 ulikuwa wa viwango tofauti. Mtiririko uliokuwa juu ya wastani ulirekodiwa katika mito ya Great Ruaha na Kilombero, wakati Mto Luwegu ulirekodi mtiririko uliokuwa chini kwa kiasi kikubwa. Jedwali la 1 linaonesha ulinganisho wa wastani wa mtiririko wa maji uliorekodiwa mwezi Agosti.


Matokeo ya Kihidrolojia

Mtiririko wa maji kuingia katika bwawa la JNHPP ulionesha kupungua taratibu kuelekea mwisho wa Agosti 2026. Pamoja na hali hiyo, kiwango cha maji katika bwawa kilibaki katika hali tulivu kwa ujumla, ingawa mwishoni mwa mwezi kilikuwa mita 0.52 chini ya wastani wa muda mrefu.




Jedwali 1: Mchanganuo wa Takwimu za Wingi wa Maji (Agosti, 2026)

Na	Namba ya Kituo	Mto	Wastani Wingi Agosti 2026 (m³/s)	Wastani Wingi wa Maji LTA Agosti 2000–2025 (m³/s)	Maelezo
1	1KA3B	Great Ruaha at Msolwa	106.95	68.76	Juu zaidi ya Wastani
2	1KB17A	Kilombero at Swero	207.9	138.66	Juu ya Wastani
3	1KC3A	Luwegu at Mbarang'andu	5.5	45.53	Chini zaidi ya Wastani



Hali ya Maji Bwawani



Kufikia mwisho wa mwezi Agosti 2026;

Kiwango cha maji katika bwawa la JNHPP kilibaki kidogo chini ya wastani wa muda mrefu wakati wa Agosti 2026, hali iliyoendana na kipindi cha ukame/msimu wa kiangazi. Hata hivyo, usimamizi madhubuti wa maji na uendeshaji wa kituo cha kuzalisha umeme uliwezesha kudumisha kiwango cha maji katika hali tulivu.

Uchambuzi

- Kufikia tarehe 31 Agosti 2026 Kiwango cha maji katika bwawa kilikuwa mita 182.35 AMSL, pungufu ya 0.52mita kutoka wastani wa muda mrefu mita 182.87 AMSL.
- Hii ni sawa na 99.72% ya wastani wa muda mrefu.
- Hali hiyo iliwezesha upatikanaji wa maji ya kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa umeme wa maji, pamoja na kukidhi mahitaji ya maji kwa matumizi mengine.

Mapendekezo

- Kuendelea na usimamizi madhubuti wa maji na uendeshaji wa bwawa ili kuhakikisha kiwango cha kutosha cha maji kinahifadhiwa kwa ajili ya uzalishaji wa umeme na mahitaji mengine ya maji.
- Kuzingatia utabiri wa mvua za El Nino unaotolewa na TMA katika kufanya maamuzi sahihi ya uendeshaji wa bwawa, usimamizi wa rasilimali za maji ili kuruhusu kiwango kitakachozidi kutolewa bila kuathiri miundombinu na wananchi waisho ukanda wa chini wa bwawa.

